**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents | Government Budget Speeches

1980-09-25

# Hotuba ya Mwl.Juliua K. Nyerere 25,SEP 1980

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/663

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

MKUTANO MKUU WA CHAMA CHA MAPINDUZI

SEPTEMBA 25, 1980

# HOTUBA YA MWALIMU JULIUS K. NYERERE

*UKUMBI WA DIAMOND JUBILEE, DAR ES SALAAM*

Ndugu Mwenyekiti, Wanachama wa CCM, na Wageni Waheshimiwa.

Naushukuru Mkutano huu, na Chama kizima, kwa kunipa Heshima hii ya kupendekezwa tena kwa Wananchi kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nilipoteuliwa, kama hivi, mwaka 1975, nilisema kwa kirefu kidogo kabla sijaukubali mzigo huu. Nilisema mambo mawili. Kwanza, nilieleza haja ya kuunganisha TANU na ASP kuwa Chama kimoja. Hilo sasa tumelifanya, na matokeo yake ni Chama cha Mapinduzi. Nchi yetu tuliyoiita Nchi ya Chama Kimoja ingawa kwa kweli ilikuwa na Vyama Viwili sasa ni Nchi ya Chama Kimoja kweli. Nadhani tuna haki ya kujipongeza kwa mafanikio hayo.

Jambo jingine nililoeleza kwa kirefu ni hatari ya kumtamka kila mara mtu yule yule kushika kiti cha Rais. Nilisema kwamba kitendo hiki cha kumteua mtu yule yule kila mara kinafanya uteuzi wenyewe uwe ni jambo la mazoea, badala ya kuwa ni jambo la kufikiriwa vizuri na kwa makini sana. Niliposema hivyo nilitaka nieleweke, na ndivyo nilivyoeleweka, kwamba sitakubali kuteuliwa kushika nafasi hii ya Urais kwa uchaguzi huu wa mwaka 1980. Na kwa kweli hiyo ndiyo iliyokuwa nia yangu, na iliendelea kuwa nia yangu mpaka hivi karibuni. Labda safari hii ni vizuri nikasema mapema kwamba naikubali tena heshima hii.

Lakini hoja nilizozitoa za kumteua mtu mwingine kugombea kiti cha Rais zilikuwa za maana mwaka 1975. Bado ni za maana mpaka sasa. Bado ni kweli kwamba "hatari moja ya kuendelea kumchagua mtu yule yule kipindi hata kipindi ni kwamba mazoea hayo huweza kuleta hofu na wasiwasi nchini". Bado ni kweli kwamba "mabadiliko ni lazima yaje maana hata kiongozi anayechaguliwa kwa maisha, hatima yake atakwenda, maana ubai una mwisho". Na ni kweli kwamba muda unavyopita uwezo wa viongozi,

wa nguvu na akili, hupunguka, na hauwezi tena kutoa aina ya huduma ambayo wananchi wanaihitaji na waliyozoea kuipata kutoka kwa mtu yule.

Hoja hizi na nyingine nilizozitoa mwaka 1975 ni hoja zinazoendelea kunilemea. Lakini ziko sababu kubwa, ambazo na mimi nazijua, za kusema kuwa, pamoja na hayo, bado mwaka 1980 siyo wakati mzuri wa kuilazimisha CCM na Taifa hili kubadilisha uongozi, ikiwa, kama mnavyosema, Chama chenyewe pamoja na Taifa, hawajayataka mabadiliko hayo.

Hali yetu ya uchumi bado ni mbaya sana. Sisi sote tunalifahamu hilo. Wananchi wanalalamika juu ya upungufu wa vitu muhimu, juu ya kupunguka kwa huduma, na juu ya magendo katika nchi yetu. Wala tusijaribu kuficha ukweli na haki ya malalamiko yao, na wajibu wetu viongozi, kuwasikiliza wananchi wanaozitoa shida hizo, na kuchukua hatua za kuzimaliza.

Lakini kwa kweli ni upuuzi kusema kwamba hali ya wananchi sasa ni mbaya zaidi kuliko ilivyopata kuwa huko nyuma. Maadui zetu tu ndio wanaotamka maneno kama hayo. Sasa hivi kuna upungufu wa sabuni kwa sababu kila mtu anataka sabuni na mara nyingi huwa anao uwezo wa fedha wa kujinunulia sabuni. Sasa hivi kuna upungufu mkubwa zaidi wa saruji kuliko wakati wo wote huko nyuma; kuna upungufu mkubwa zaidi wa mabati kuliko wakati wo wote huko nyuma. Watu wengi zaidi wananung'unika kwa sababu ya upungufu wa saruji na mabati kuliko wakati wo wote huko nyuma; kwani sasa hivi watu wengi zaidi wanataka kujenga na wanao uwezo wa kujenga nyumba za kudumu kuliko wakati wo wote huko nymua. Na vivyo hivyo kwa vitu kama mafuta ya taa, mafuta ya kupikia, sukari, nyama. Na vivyo hivyo kwa huduma za umma kama madawa, shule, vitabu, karatasi, usafiri wa reli, mabasi, na kwa wananchi wenye uwezo zaidi, hata usafiri wa ndege. Miaka ishirini, miaka kumi, au hata miaka mitano iliyopita, hali haikuwa hivyo. Bidhaa hizo na, huduma hizo hazikuwa vitu vya kawaida majumbani mwetu au wilayani mwetu wakati wa uhuru. Wakati tulipo-adhimisha miaka kumi ya uhuru mwaka 1971, bidhaa hizo

na huduma hizo hazikuwa za kawaida majumbani kwetu. Hazikuwa za kawaida wala za kutazamiwa katika kaya zetu wakati wananchi walipokuwa wanaishi mmoja mmoja, kabla ya kuhamia vijijini.

Lakini sasa bidhaa hizo zinatazamiwa ziwepo; na sasa zikikosekana watu wetu wanaona kuwa wamepungukiwa; na serikali inatambua kwamba ni vibaya ikiwa bidhaa hizo na huduma hizo hazipatikani kila mahali vijijini na mijini. Zote hizo ni dalili za hatua ya maendeleo tuliyopiga. Vile vile ni kipimo cha matokeo ya vijiji, ya UPE, ya kuenezwa kwa huduma za msingi za afya na kwa huduma za usafiri. Kutokana na vitendo vya TANU, ASP, CCM na vya Serikali, sasa watu wetu hawakubali tena kusema kuwa umasikini na upungufu wa vitu ni amri ya Mungu. Na kuukataa umaskini na unyonge ni hatua ya kwanza ya kuushinda umaskini na unyonge huo, ikiwa njia za maendeleo zi wazi, na wananchi wanaelewa jinsi ya kuyatafuta maendeleo hayo. Hatua hii nayo inahitaji uongozi na utaratibu.

Lakini pamoja na maelezo hayo, ya kwamba matatizo tuliyonayo ni matatizo ya maendeleo, ukweli unabaki pale pale kwamba, wananchi sasa wanatazamia kuzipata bidhaa hizi muhimu na kwamba uchumi wetu sasa hivi hauwezi kutengeneza bidhaa hizo kwa kiasi cha kutosha. Haiwezekani kufanya hivyo kwa sababu hakuna uwezo wa kutengeneza kiasi cha kutosha cha bidhaa za kutumia wenyewe na kuuza nje. Na hasa fedha za kigeni tunazozipata hazitoshi kulipia vitu vyote ambavyo bado tunavihitaji kutoka nje, pamoja na vifaa na spea za viwanda vyetu tulivyovijenga katika miaka hii michache iliyopita. Njia ya kuondoa upungufu huu sasa ni kuongeza kilimo na utengenezaji wa bidhaa za viwandani ili tuongeze fedha za kigeni tunazopata kutokana na mauzo ya vitu hivyo.

Kama, mpaka sasa, matatizo haya yangekuwa yanatokana na siasa yenyewe ya Chama chetu, au Serikali kushindwa kuitekeleza vizuri siasa hiyo, au makosa ya uongozi, basi dawa inayofaa katika Kikao hiki ingekuwa wazi kabisa. Dawa nyepesi ingekuwa ni kubadili Rais wa Jamhuri, na pengine hata kubadili mipango ya Chama.

Kwa bahati mbaya dawa ya matatizo yetu si rahisi kiasi hicho. Ukweli ni kwamba matatizoyetu ya sasa hayakuja kwa sababu ya siasa yetu ya ujamaa, au hata kwa sababu ya uzembe. Ni kweli kabisa kwamba uzembe nao umefanya hali yetu kuwa mbaya zaidi; wala sitaki nidhaniwe nasema kwamba uongozi wetu au utekelezaji wetu usingekuwa bora zaidi kuliko ulivyokuwa. Lakini ukweli wa msingi ni kwamba duniani kote nchi maskini zisizokuwa na mafuta zote zina matatizo makubwa sana ya uchumi, bila ya kujali siasa zao za ndani au ufanisi wao wa utekelezaji. Tofauti ya ujamaa na siasa nyingine ni katika kuyagawana matazizo hayo kwa usawa miongoni mwa raia wake; lakini hakuna tofauti katika matatizo yenyewe. Nchi maskini za kibepari na nchi maskini za kijamaa, zote zimo katika hali ile ile. Zote zina matatizo makubwa mno ya fedha za kigeni hata haziwezi tena kuagiza kutoka nchi za nje bidhaa muhimu za kuendesha uchumi wao. Kuhangaikahangaika katika kulitatua tatizo hili ndiko kunakofanya baadhi ya nchi maskini kuuza kidogo uhuru wao wa kujiamulia mambo ili wapate chakula au misaada ya fedha. Na baadhi ya nchi hizo zimekwisha kugundua kwamba, hata kwa kufanya hivyo, nafuu inayopatikana ni ya muda mfupi tu, na baada ya hapo tatizo lenyewe linawaelemea tena.

Sikusudii kuzungumza juu ya matatizo ya uchumi wetu hivi sasa; matatizo hayo nilikwisha kuyazungumza Bungeni Julai 22 mwaka huu, na sina shaka tutaendelea kuyazungumza. Nayataja matatizo haya kwa sababu nimesikia na kuelewa minong'ono ya Wananchi, kwamba kwangu mimi kukataa mwenyewe uongozi wa taifa hili kwa wakati huu ni sawa na kukataa kutimiza wajibu. Ni sawa na kukimbia kutoka uwanja wa mapambano na huku vita bado vinaendelea. Maana tunakabiliwa na mapambano ya vita vya uchumi wetu. Uchumi wa taifa bado unaendelea kuuguza majeraha yaliyotokana na vita tulivyolazimishwa kupigana. Kwa kweli ni kana kwamba vita vile bado vinaendelea katika hali nyingine.

Si rahisi kupuuza minong'ono hii, na wala haina maana kusema kuwa maoni haya hayana uzito. Katika hali yetu ya sasa ni wajibu wa kila mmoja wetu, hapo alipo, kufanya

kila analoweza kulivusha Taifa letu kutokana na matatizo haya. Kubadili nahodha si jambo baya, lakini kama si lazima kabisa kufanya hivyo basi si vibaya kusubiri mpaka mawimbi yakatulia kidogo.

Tunalo tatizo la pili. Tatizo hili ni kwamba mpaka sasa hatuna utaratibu mzuri wa kubadili ama kiongozi wa Chama chetu, au Rais wa Jamhuri. Na tatizo hili linatokana na historia ya vyama vyetu vya zamani.

Chama cha TANU kilikuwa na tabia ya kuchagua viongozi wake. Kwa muda mrefu, kabla na baada ya uhuru, kilikutana kila mwaka na kufanya uchaguzi wa Viongozi. Mara nyingi viongozi wengi walibadilishwa, tangu Matawini, Wilayani, Mikoani na katika ngazi za Taifa. Viongozi wa Chama katika Kamati Kuu au Halmashauri Kuu ya Taifa hawakuendelea kuchaguliwa mwaka hata mwaka kama masultani. Kadhalika Wabunge wamekuwa wakichaguliwa katika vipindi maalum na katika kila uchaguzi kulikuwa na mabadiliko.

Kwa mfano. Mwaka 1974 Tanzania Bara ilikuwa na Wenyeviti wa Wilaya 85, na baada ya kuongeza Wilaya wakawa 96. Baada ya kuunganisha vyama tulifanya uchaguzi mpya. Wenyeviti wa zamani waliochaguliwa tena walikuwa 33. Wengine ama hawakugombea kiti, ama waligombea lakini hawakuchaguliwa.

Vile vile, mwaka 1974 Tanzania Bara walikuwako Wenyeviti wa Mikoa 20. Tulifanya uchaguzi wa CCM, sita hawakugombea viti. Katika 14 waliogombea, sita walichaguliwa tena; waliobaki hawakuchaguliwa.

Kwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu, wanaochaguliwa na Mkutano huu, katika wale 20 waliokuwapo mwaka 1974, wanane hawakugombea viti. Katika 12 waliogombea, wanane walichaguliwa tena katika uchaguzi wa 1977 na wanne hawakuchaguliwa.

Kwa Wabunge vile vile. Kati ya Wabunge 107 wa kuchaguliwa waliokuwako katika Bunge la 1965, Wabunge 74 waliamua kugombea viti tena katika uchaguzi

wa 1970. Kati ya hao, 16 hawakuteuliwa na Chama katika vikao vya Wilaya. Wanachama wengine wa TANU waliteuliwa kugombea viti hivyo. Kwa hiyo ni wana-TANU 58 tu kati ya wale waliochaguliwa katika Bunge la 1965 ndio waliorudi tena kwa wananchi kutaka wachaguliwe. Kati ya hao, 36 walichaguliwa wakawa Wabunge tena; wengine hawakuchaguliwa. Ndiyo kusema kwamba katika jumla ya wale 74 walioamua kugombea viti vya ubunge ni 36 ndio walioweza kurudi Bungeni. Na katika uchaguzi wa 1975, Wabunge wa zamani 86 walijaribu kuchaguliwa tena, hatimaye 43 kati yao wakachaguliwa kuwa Wabunge katika kipindi cha 1975-1980.

Kwa hiyo, kwa Tanzania Bara, TANU ilijenga utaratibu na tabia ya kuchagua na, kama hapana budi, kubadili viongozi wake wa ngazi zote hizo. Hofu haikuwa kwamba viongozi hao wangeweza kuendelea kama masultani; hofu ya kweli ilikuwa kwamba tungeweza kujenga tabia mbaya ya kubadili-badili viongozi kila msimu kama kina mama wanavyobadili kanga na vitenge. Lakini hata hofu hiyo, ingawa ipo, na ni kubwa zaidi kuliko hofu ya usultani, si hofu kubwa mno. Yako mazoea ya kubadili viongozi; lakini pia iko tabia ya kuendelea na viongozi ambao wanachama na wananchi kwa jumla wanaendelea kuridhika na uongozi wao. Tunao Wabunge waliomo Bungeni tangu mwaka 1960.

Kwa Tanzania Visiwani ASP, kwa sababu mbalimbali haikujenga utaratibu na tabia ya kuchagua viongozi wake mara kwa mara na kwa vipindi maalum. Baada ya Mapinduzi ya Januari 1964, kulikuwa kuna sababu ya nyongeza ya kutofanya uchaguzi wa viongozi wa Chama wala serikali. Kwa kweli yakaanza kutamkwa mawazo kwamba uchaguzi wa viongozi si jambo jema, siyo kwa wakati huo tu wa matatizo ya mapinduzi, lakini kwa wakati wo wote. Kwa hiyo ASP haikujenga utaratibu wala tabia ya kuchagua viongozi wake kwa ngazi yo yote. Katika hilo walikuwa na tofauti kubwa na TANU.

Lakini katika uchaguzi wa Kiongozi Mkuu wa Chama na Serikali ingawa kulikuwa na tofauti ya nadharia hapakuwa na tofauti kubwa ya mazoea. Wanachama wa

ASP hawakukutana kila baada ya kipindi fulani kwa ajili ya uchaguzi wa Kiongozi wake Mkuu. Viongozi wa TANU walikutana kila mwaka, na baadaye kila baada ya miaka mitano, kufanya hivyo. Lakini kila walipokutana walimchagua kiongozi yule yule. Kwa hiyo ASP waliendelea kuwa na Kiongozi yule yule na TANU waliendelea kuwa na Kiongozi yule yule. Kwa ngazi ya Kiongozi wa juu hata TANU hawakujenga utaratibu na mazoea ya kubadili Kiongozi wao.

Sasa tunacho Chama kimoja, CCM. Chama hiki kimeunda utaratibu wa kuchagua viongozi wetu Bara na Visiwani. Utaratibu huo ndio tunaoutumia hivi sasa kuchagua viongozi wa ngazi mbali mbali wa Chama na Serikali. Lakini CCM, mpaka sasa, haina utaratibu wa kubadili Kiongozi wake wa juu, ambaye sasa ana kofia zote mbili, ya Chama na ya Serikali.

Huku kutokuwa na utaratibu na tabia ya kubadili ni sababu nyingine ya kutotumia wakati huu kubadili kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Muda wa miaka mitano iliyopita tungeweza kuwa tumeutumia kutengeneza angalau utaratibu wa kubadili Rais wa Jamhuri. Lakini kwa bahati mbaya, na pengine kwa sababu ya shughuli na matatizo mengi ya kipindi hicho, hatukufanya hivyo.

Sababu hizi mbili, hali ya uchumi wetu kwa sasa, na haja ya kuandaa utaratibu wa mabadiliko kabla ya kufanya mabadiliko yenyewe, ndizo zilizonifanya nikakubali pendekezo la Halmashauri Kuu, na sasa pendekezo lenu, kwamba Chama kipendekeze jina langu kwa Wananchi ili, wakiafiki, niendelee kwa muda kuwa Rais wa Jamhuri yetu.

Katika sababu hizi mbili ni dhahiri kwamba ingawa haionekani hivyo, sababu kubwa ni hii ya pili, yaani haja ya kuandaa utaratibu na mawazo yetu kwa mabadiliko ambayo lazima tuyafanye kwa faida ya Nchi yetu.

Matatizo ya uchumi yako ya aina mbili. Kwanza tunayo yale ya muda mrefu na ambayo yanazikabili nchi zote zinazoendelea. Pili tunayo haya ya muda mfupi, yaliyotokana

na mafuriko na ukame na vita, ambayo ni yetu tu. Ni dhahiri kwamba matatizo tunayoyasema ni haya ya muda mfupi, si yale ya muda mrefu. Maana tukiyafanya hayo ya muda mrefu kuwa ni sababu ya kutobadili Rais wa Jamhuri, basi tungelazimika kuchagua Rais wa Maisha. Kwa kweli, kama tungekuwa tumejiandaa vizuri kabisa kwa mawazo na kwa utaratibu, hata matatizo haya ya uchumi ya muda mfupi yasingekuwa sababu ya kutosha ya kutobadili Rais wa Jamhuri wakati huu.

Kwa hiyo nasema nini? Nasema tunazo sababu mbili za kutufanya tusibadili Rais wa Jamhuri, kama hivyo ndivyo wananchi wanavyotaka. Sababu zote mbili ni za muda, na ya maana zaidi ni ile ya kujiandaa, kabla ya kuleta mabadiliko yenyewe.

Kwa hiyo, ikiwa nitachaguliwa tena, kazi moja ambayo itanibidi nisaidiane na wenzangu kuifanya ni kufanya mabadiliko ya maandalizi ya kubadili Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Nitataja baadhi ya mabadiliko ambayo nadhani itafaa tuyafanye katika jitihada zetu za kuandaa utaratibu wa mabadiliko.

Kwanza, nadhani ni vizuri tumwondolee Rais, au mwananchi mwingine, au Kikao cho chote cha Chama au Serikali, mzigo wa kuamua na kutamka kwamba wakati wa Rais kung'atuka umefika. Si vizuri Rais mwenyewe afanye, au atazamiwe kufanya, uamuzi na tamko la kuacha kiti chake. Nayaona matatizo yake. Na wala si vizuri uamuzi huo ufanywe au utazamwe kufanywa na mtu ye yote au Kikao cho chote cha Chama chetu au Serikali. Inaweza ikawa vigumu kabisa kwa mtu ye yote au Kikao cho chote cha Chama au Serikali kufanya uamuzi huo au tamko hili. Kwa kweli tunaweza tukafikia mahali ambapo kwa mtu ye yote au kikao cho chote kuamua hivyo kutadhaniwa ni utovu wa heshima kwa Rais wa Jamhuri, na usaliti kwa nchi yetu. Tamko hili ni vizuri liingizwe ndani ya Katiba yenyewe. Ni vizuri Katiba iseme, kwa mfano, kwamba Rais anaweza kushika madaraka hayo kwa vipindi viwili vya

miaka mitano-mitano. Kila wakati tutajua kwamba, baada ya muda usiozidi miaka kumi, tutakuwa hatuna budi kuchagua Rais mpya. Hili litakuwa ni badiliko la Katiba na la kudumu.

Pili, nadhani ni vizuri tufanye utaratibu wa kushirikisha Matawi yote ya Chama katika shughuli za awali za kuangaa-angaa na kutaja majina ya Wanachama wa CCM ambao wangeweza kufikiriwa kushika madaraka ya Urais wa Jamhuri. Utaratibu huo nao unaweza ukawa wa kudumu, lakini si lazima uwe wa Katiba; unaweza ukawa utaratibu wa mazoea tu.

Tatu, nadhani kwamba pana haja ya kufanya badiliko moja ambalo si lazima liwe la Katiba wala la kudumu. Sasa Rais wa Jamhuri ndiye pia Mwenyekiti wa CCM. Tungeweza tukazitenga kofia mbili hizi angalau kwa muda. Tungeweza kuwa na kipindi kifupi cha mabadiliko ambapo Rais wa Jamhuri na Mwenyekiti wa CCM ni watu wawili mbali mbali. Badiliko hili lingekuwa kama daraja la muda mfupi, la kutuvusha kutoka kule ambako tulikuwa hatubadili Rais wa Jamhuri kwenda kule ambako tunaanzisha taratibu na mazoea ya kufanya hivyo.

Nasema badiliko hili si vema liwe la Katiba, au la kudumu, kwa sababu, ingawa naamini kabisa kwamba tabia hii ya kushika kofia mbili inaweza kuathiri uhai wa Chama, nadhani yako maeneo ambako ni vizuri kuendelea kuzichanganya kofia hizi; na eneo moja ni la Mwenyekiti wa Chama na Rais wa Jamhuri.

Ndugu Mwenyekiti. Kwa mara ya pili nimetoa hotuba ndefu katika kukubali heshima niliyopewa na Mkutano huu. Nimefanya hivyo kwa sababu nataka Chama, na nchi nzima, ielewe kwa nini kwa muda mrefu nimekuwa nasita kuipokea heshima hii tena, na ielewe vile vile kwa nini nimebadili mawazo. Nilisema mapema kabisa katika hotuba hii kwamba naikubali heshima hii. Naikubali kwa wingi wa heshima na Shukurani kwa Mkutano huu na Chama chetu kwa jumla.

Lakini pamoja na shukurani hizo ni wajibu wangu, na pia ni heshima kwa Chama chetu na Wananchi wote kwa jumla, kutamka wazi wazi safari hii, kwamba naikubali heshima hii kwa mara ya mwisho.

Nasema hivyo kwa sababu pamoja na sababu hizo zilizonifanya nibadili mawazo na niikubali tena heshima hii, naendelea kuamini kwa dhati kabisa kwamba katika hatua ambayo Taifa letu sasa limeifikia, haja ya kubadili uongozi ni kubwa zaidi kuliko haja ya kuendelea na uongozi ule ule katika ngazi ya Urais. Matatizo yanayoweza kutokana na kubadili Rais ni madogo zaidi kuliko matatizo yanayoweza kutokana kuwa na Rais yule yule kwa kipindi kingine kirefu. Hatua zetu za awali za kujenga demokrasi zitakuwa zimekamilika hapo tutakapokuwa tumetayarisha taratibu za kubadili Rais wa Jamhuri na kuzitumia bila mgogoro. Kwa sababu ya wasiwasi uliopo juu ya mabadiliko, na kwa sababu hapo yatakapokuja yatakuwa ni jambo geni, itakuwa vizuri kama wote tutashirikiana katika kuyatekeleza mabadiliko hayo. Si jambo jema kwa Taifa letu kama tukiichelewesha mno hatua hii.

Ndugu Mwenyekiti, namaliza kama nilivyoanza.

Nawashukuru wote kwa Imani hii mpya mliyoionyesha kwangu, nami nitajitahidi kuiheshimu Imani hiyo. Na nawashukuru pia kwa kunisikiliza kwa utulivu.